# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
# CHUO CHA UALIMU SONGEA

**Anuani**: Chuo cha Ualimu Songea
**Simu**: 0759172182
**e-mail:** songeatc@moe.go.tz
Tovuti: www.songeatc.ac.tz

S.L.P 189
**SONGEA;**
**RUVUMA.**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na**. STC/A/1/VOL.VIII/52** Tarehe: **30/05/2025.**

**Ndugu ……………………………………….................**

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU MWAKA 2025/2026</u>**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu kozi ya Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi katika Chuo cha Ualimu Songea. **Hongera Sana.**

Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi na Hisabati ni kozi ya miaka **mitatu (3**) kwa wahitimu wa kidato cha nne. Ufafanuzi zaidi kuhusu masomo na mitihani yatatolewa wakati wa maelekezo kabilishi (Orientation Course) ambayo yatatolewa kwa wanachuo wote wiki ya kwanza baada ya kuripoti chuoni. Lengo la mafunzo ni kukuandaa kuwa mwalimu mahiri na mwenye ujuzi stahiki ili uweze kufundisha kwa ufanisi katika Shule ya Msingi nchini.

## 2.0 MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo Songea mjini, mtaa wa Matogoro Shuleni, umbali wa kilometa 4 kutoka stendi ya zamani ya mabasi Songea mjini, upande wa Mashariki kufuata barabara iendayo Tunduru. Kwa unayetokea barabara ya Njombe unashauriwa kushuka Kituo kikuu cha mabasi Songea (**Shule ya tanga**) kisha panda daladala hadi stendi ya mabasi Songea mjini. Usafiri wa taxi kutoka Songea mjini kuja chuoni gharama haizidi Tshs 10,000/=. Kwa unayetokea barabara ya Tunduru shuka stendi ya mabasi **SeedFarm** na usafiri wa taxi haizidi Tshs.5,000/=. Aidha, usafiri wa Bodaboda unapatikana kwa gharama ya Tshs 1,000/= hadi 2,000/=.

## 3.0 DIRA, SHABAHA NA KAULI MBIU

### 3.1 DIRA (VISION)

'Kuwa chuo bora cha mafunzo ya ualimu kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia ili kupata walimu wenye maadili, kujituma na mahiri watakaohudumia jamii ndani na nje ya nchi'.

### 3.2 SHABAHA (MISSION)

'Kuandaa walimu wenye maarifa ya kutosha, mbinu bora za kufundishia, uwezo wa kuendesha tafiti za kielimu na masuala mtambuka'.

**3.3 KAULIMBIU:** Kaulimbiu yetu ni **"Angaza Umma"**

## 4.0 TAREHE YA KUFUNGUA CHUO

Chuo kitafunguliwa Tarehe **14/07/2025** kwa ajili ya usajili na kuanza rasmi masomo. Usiporipoti chuoni ndani ya wiki mbili unaweza kupoteza nafasi yako.

## 5.0 MAWASILIANO

Iwapo Mzazi au Mlezi anahitaji kuwasiliana na Uongozi wa Chuo atumie namba hizi: **0759172182** au **0759168813**

## 6.0 MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

Ili uweze kusajiliwa unapaswa kuja na mahitaji muhimu, vyeti na vitambulisho kama ifuatavyo:

i. Vyeti halisi (**Original certificates**) vya kufuzu kidato cha nne na vyeti vya kidato cha sita kwa wale waliohitimu kidato cha sita (nakala tatu kwa kila cheti)
ii. Cheti halisi cha kuzaliwa (**Original birth certificate**) na nakala zake tatu;
iv. Fomu ya afya **(Medical Examination Form)** iliyojazwa na Mganga wa hospitali inayotambuliwa na Serikali;
v. Picha **tatu (03)** passport size zenye background rangi ya buluu bahari na picha nzima **(full photo)** moja (1) yenye background ya buluu bahari uliyopiga ukiwa umevaa sare ya Chuo.

**Muhimu:** *Usipoleta **vyeti halisi** hutasajiliwa; hivyo utalazimika kufuata vyeti nyumbani*

## 7.0 ADA YA MAFUNZO NA MICHANGO MBALIMBALI

### 7.1 ADA

Ada ya mafunzo ni Tshs.**450,000/=** kwa mwaka (TShs.**225,000/=** kwa muhula). Lipa mara baada ya kupewa namba ya kumbukumbu ya malipo ya serikali **(Control Number)** na Mhasibu wa Chuo. Aidha, unaweza kuomba "Control Number" na ukalipa ada ukiwa nyumbani kwa kupiga simu zilizopo kwenye kipengele **Na.5.** Hakikisha umelipa ada yote 450,000/= au nusu 225,000/= mwanzo wa muhula (wakati au kabla ya kuripoti chuoni).

## 7.2 MICHANGO MBALIMBALI

| NA. | MCHANGO | KIASI (Tshs.) | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1. | Serikali ya Wanachuo (SEWASO) | **5,000/=** | Kwa mwaka |
| 2. | Huduma ya kwanza | **10,000/=** | Kwa mwaka |
| 3. | Usafi na Mazingira | **20,000/=** | Kwa mwaka |
| 4. | Kukodi Godoro | **10,000/=** | Kwa mwaka |
| 5. | Usajili na Kitambulisho | **20,000/=** | Kwa mwaka |
| 6. | Michezo | **30,000/=** | Kwa mwaka |
| 7. | Ulinzi | **30,000/=** | Kwa mwaka |
| 8. | Ukarabati | **25,000/=** | Kwa mwaka |
| 9. | Bima ya Afya (NHIF) | **50,400/=** | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **200,400/=** | |

Malipo ya michango yafanyike kupitia akaunti zifuatazo:

**1.** Mchango wa SEWASO Tshs **5,000/=**
Jina La Akaunti: **SEWASO**
Akaunti Namba: **61802300189** iliyopo Benki ya **NMB**

**2.** Michango Mingine Iliyobaki Tshs **195,400/=**
Jina la Akaunti: **Songea Teachers' College Miradi Account**
Akaunti Namba: **61801100014**
Benki: **NMB**

**Muhimu:** Lipa Ada na Michango mwanzo wa muhula na siyo vinginevyo. Usipolipa ada na michango hutasajiliwa.

## 8.0 SARE YA CHUO

### 8.1 WAVULANA

i. **Suti nyeusi moja na suti ya buluu nyeusi moja (dark blue):** Suruali zenye zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up) **sentimeta 16 hadi 18.** Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku ya alhamisi na ijumaa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi (Rejea picha Na.1). Mshono wa Koti la suti uwe na kifungo kimoja (1) au viwili (2) kama unavyoonekana katika picha Na. 5**;**
ii. **Shati mbili (2)** za mikono mirefu, rangi ya **'Light blue'** (Rejea picha Na. 3);
iii. Tai ndefu mbili (**02**), nyeusi na buluu nyeusi;
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa Kamba (Buti haziruhusiwi)
v. Soksi nyeusi ndefu angalau jozi 4;
vi. Mkanda wa suruali wa ngozi rangi nyeusi;
vii. T-Shirt inapatikana chuoni kwa gharama ya **Tsh 15,000/=.**

**8.2 WASICHANA**

i. **Suti nyeusi moja na suti ya buluu nyeusi moja (dark blue):** Sketi za rinda boksi za heshima zenye urefu wa sentimeta 15 hadi 25 kutoka kwenye goti kuelekea miguuni. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa siku ya alhamisi na ijumaa (Rejea picha Na. 2); Mshono wa Koti la suti uwe na vifungo viwili (2) au vitatu (3) kama unavyoonekana katika picha Na.4

ii. **Shati mbili (2)** za mikono mirefu, rangi ya **'Light blue'** (Rejea picha Na.3);

iii. Tai ya kipepeo rangi nyeusi na buluu nyeusi;

iv. Kwa Waislamu mnaruhusiwa kuvaa Hijab rangi ya **'light blue'**, (kama yalivyo mashati);

v. Viatu vyeusi vya kufunika vyenye kisigino kifupi na kipana ("Simple Shoes" haviruhusiwi).

vi. Soksi nyeupe ndefu angalau jozi nne (4);


vii. T-Shirt inapatikana chuoni kwa bei ya Tshs **15,000/=.**

**Muhimu:**


i. Mavazi yako yote kwa wakati wote ni **LAZIMA** yaakisi maadili bora ya Ualimu. Nguo za kubana, pensi, vimini/vitop au nguo zenye mipasuo mikubwa na mavazi angavu hayaruhusiwi.

ii. Sare za **kuteleza/mtelezo** na **mitumba** haziruhusiwi.

iii. Uje na nguo chache za kushindia zisizozidi **jozi nne (4)**




Picha Na.1




Picha Na.2



Picha Na.3



**Picha Na.4**



**Picha Na.5**

**9.0 NGUO ZA MICHEZO**

i. T-shirt na bukta rangi ya buluu,
ii. Track-suit moja (1) rangi ya buluu,
iii. Raba nyeusi jozi moja (1).

**10.0 MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI**

i. Mashuka mawili (2), rangi ya pinki,
ii. Blanketi moja (1),
iii. Chandarua rangi nyeupe,
iv. Mto na foronya rangi ya pinki,
v. Ndoo mbili (2) za lita 10.

**11.0 Vyombo vya Chakula**

Sahani, bakuli, kikombe na kijiko. Vyombo vya plastiki haviruhusiwi.

**12.0 MAHITAJI YA KITAALUMA NA MITHANI**

i. Daftari kubwa quire 3 angalau kumi (10),
ii. Mihutasari (Syllabus) ya masomo yanayofundishwa shule ya Msingi,
iii. Vitabu (Kiongozi cha Mwalimu na vitabu vya kiada) vinavyoakisi mtaala wa elimu ya msingi uliboreshwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) mwaka 2023,
iv. Scientific calculator f(x) 991,
v. Mathematical set,
vi. Kalamu ya wino na penseli za kutosha,
vii. Koti jeupe (Laboratory Coat) kwa matumizi ya maabara,
viii. Rimu moja (1) ya karatasi nyeupe (A4) kwa mwaka,
ix. Fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Mitihani Ths **20,000/=** kwa mwaka.

**13.0 AFYA**

Unaelekezwa kuzingatia yafuatayo kwa ajili ya ustawi wa afya yako kwa kipindi chote cha mafunzo:

i. Uje na fomu ya afya (iliyoambatanishwa) ikiwa imejazwa kikamilifu na mganga wa hospitali ya serikali kwa uthibitisho wa afya yako;
ii. Chuo hakitoi chakula maalumu (***Special diet****);*
iii. Iwapo una kitambulisho cha **Bima ya Afya (NHIF)**, uje nacho kwa ajili ya matibabu. Mwanachuo usiye na Bima ya afya unapaswa kulipa **Tshs 50,400** kwa ajili ya kujiunga na mpango wa Bima ya Afya kwa wanafunzi. Taratibu za kujiunga na Bima ya Afya zitaratibiwa na chuo kwa kushirikiana na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

**14.0 VIFAA VYA USAFI**

Elimu bora hutolewa katika mazingira safi na salama. Hivyo basi, unapaswa kuleta **Fyekeo 1** ambalo litatumika kwa shughuli za usafi katika mazingira ya chuo.

## 15.0 MAHAFALI

Chuo kina utaratibu wa kufanya mahafali ya kuwaaga wahitimu wa mafunzo ya Ualimu kila mwaka. Hivyo basi kufanikisha mahafali hayo, unapaswa kuchangia Tshs.**10,000/=** Kwa mwaka.

## 16.0 SHERIA NA KANUNI ZA MWENENDO BORA WA MWANACHUO

Wanachuo wote huongozwa kwa sheria na kanuni za mwenendo bora wa mwanachuo. Hivyo, unashauriwa kusoma kwa makini na kuzielewa sheria na kanuni za mwenendo bora wa mwanachuo ambazo zimeambatishwa pamoja na fomu hii.

## 16.0 MWISHO

Ualimu bora huanzia chuoni kwa mwanachuo kuonesha **nidhamu, kujituma katika masomo na kazi za nje ya darasa.** Jumuiya ya Chuo cha Ualimu Songea inakutakia maandalizi mema na Safari njema ya kuja Chuoni.

**Karibu sana Chuo cha Ualimu Songea**

......................................

**Catherine T. Kimboka**

**Mkuu wa Chuo**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU SONGEA
S L.P. 189
SONGEA

## GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

From: The Principal,
Songea Teachers
College,
P. O. Box 189,
**SONGEA.**

TO: The Medical Officer
……………………………………..……………………

**RE: …………………………………………………....(STUDENT NAME IN FULL)**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

1. Eye disorder
2. Ear, Nose/Throat disorder
3. Speech
4. Venereal Diseases
5. Leprosy
6. Limbs
7. Epilepsy
8. Asthma
9. Blood Group
10. Pregnancy
11. Any other serious diseases

Signature ……………
MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU SONGEA
S.L.P. 189
SONGEA

Date: **30/05/2025**

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by **Government Medical Officer**)

I have examined the above named student that he/she is physically *fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time Teacher Education course.

1. Eye disorder……………………………………………………………………………………
2. Ear, Nose/Throat disorder…………………………………………………………………………
3. Speech ……………………………………………………………………………………
4. Venereal Diseases ………………………………………………………………………
5. Leprosy ……………………………………………………………………………………
6. Limbs ……………………………………………………………………………………..
7. Epilepsy ……………………………………………………………………………………
8. Asthma ……………………………………………………………………………………
9. Blood Group
   …………………………………………………………………………………………….
10. Pregnancy ……………………………………………………………………………………
11. Any other serious diseases……………………………………………………………………

Name…………………………….…………Designation …………………. Signature ………………

Date ……………………………… Official Stamp:

***Delete whichever inapplicable**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU SONGEA**

# SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA MWENENDO BORA WA MWANACHUO

## 1.0 UTANGULIZI

Miongozo na taratibu za mafunzo ya ualimu zinalenga kuwaandaa walimu wenye mtazamo, tabia na uelekeo wa taaluma ya ualimu. Mtazamo, tabia na uelekeo mzuri hujengwa na kukuzwa kutokana na matendo mema, na matendo mema huakisi utii wa kanuni na taratibu zinazoongoza. Kanuni na taratibu zifuatazo zitawezesha uendeshaji na usimamizi wa mafunzo ya ualimu kwa wanachuo kwa kiwango cha juu cha ufanisi na ubora.

## 2.0 UTII WA SHERIA ZA NCHI NA ALAMA ZA TAIFA

**2.1** Mwanachuo atawajibika kutii na kuzifuata Sheria za nchi.

**2.2** Mwanachuo atawajibika kuzitii Alama za Taifa kama vile Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.

**2.3** Mwanachuo hataruhusiwa kwa namna yoyote ile katika mazingira yoyote yale kufanya udanganyifu ikiwa ni pamoja na kughushi nyaraka za kiserikali, kielimu au kiofisi.

**2.4** **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 2.1 – 2.3 sambamba na kuchukuliwa hatua kwa utaratibu uliowekwa na Sheria za nchi, atastahili adhabu ya papo kwa papo ambayo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/ kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa makosa kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

## 3.0 HESHIMA NA UTII

**3.1** Mwanachuo ajiheshimu mwenyewe, awaheshimu wenzake, wafanyakazi na watu wengine anaokutana nao. Salamu itolewe kwa heshima kwa kuzingatia utamaduni na maadili ya Kitanzania.

**3.2** Mwanachuo awe na lugha yenye hadhi ya taaluma ya ualimu na matendo yake yawe yanakuza heshima na utu wake. Aidha, lugha zinazoruhusiwa kwa mawasiliano hapa chuoni ni Kiswahili na Kiingereza.

**3.3** Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufuata ratiba ya Chuo na shughuli zinazoambatana na ratiba.

**3.4** Mwanachuo anapaswa kuwa mtiifu kwa kengele au ishara nyingine yoyote itakayomhitaji kufika mahali anapotakiwa.

**3.5** Mwanachuo sharti awahi wakati wote anapohitajika chuoni mfano: kuripoti chuoni, mstarini, bwaloni, ukumbini, darasani, katika kazi za nje na mahali pengine.

**3.6** Mwanachuo haruhusiwi kujihamisha bweni au chumba alichopangiwa. Aidha kwa namna yoyote ile mwanachuo haruhusiwi kulala bweni ambalo hakupangiwa.

**3.7** Mwanachuo haruhusiwi kufanya udanganyifu na au upotoshaji wa taarifa wa aina yoyote kwa jambo lolote wakati wote wa mafunzo.

**3.8** **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 3.1 – 3.7 atafunguliwa mashtaka na kupewa adhabu ya papo kwa papo na kiongozi wa serikali ya wanachuo, mkufunzi au Mratibu wa masuala ya wanachuo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

## 4.0 MAHUSIANO

**4.1** Mwanachuo wa kike haruhusiwi kwenda bweni la wanaume na mwanachuo wa kiume haruhusiwi kwenda bweni la wanawake bila idhini maalum kutoka ofisi ya uratibu wa masuala ya wanachuo.

**4.2** Mahusiano kati ya wanachuo, walezi na jamii yanapaswa kuwa ya kuheshimiana. Wanachuo walio kwenye ndoa watoe uthibitisho wa cheti cha ndoa kwa Mratibu wa masuala ya wanachuo na wafuate kanuni na taratibu za Chuo.

**4.3** Mahusiano ya kingono na mtu yeyote hayaruhusiwi.

**4.4** Mwanachuo anaruhusiwa kutembelewa au kupokea mgeni siku za mwisho wa wiki au sikukuu na sio siku za masomo. Mwanachuo anaelekezwa kuongea na mgeni wake katika maeneo yatakayoruhusiwa na Chuo. Wageni wanaruhusiwa kuingia chuoni kuanzia saa 5:00 asubuhi na kuondoka chuoni kabla ya saa 11.00 jioni.

**4.5** Mgeni wa dharura wa mwanachuo (atakayekuja chuoni siku za masomo) aelekezwe kuonana na Mratibu wa masuala ya wanachuo.

**4.6** Mgeni wa mwanachuo haruhusiwi kutembelea au kupumzika katika mazingira ya Chuo pasipo ruhusa ya Uongozi wa Chuo.

**4.7** Mwanachuo haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mtumishi yeyote bila ruhusa maalumu kutoka kwa Mratibu wa Masula ya Wanachuo.

**4.8** **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 4.1 – 4.8 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea**

**mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

**5.0: USAFI, AFYA NA MAZINGIRA**

5.1 Mwanachuo anaelekezwa kuoga kila siku na kuweka mwili wake katika hali ya usafi wakati wote.

5.2 Mwanachuo anatakiwa kuwa na nywele fupi zisizozidi urefu wa sentimeta moja (sm 1) na zinazotunzwa vizuri kwa kuoshwa na kuchanwa. Aidha, wasichana watakaopenda kusuka nywele wanaelekezwa kusuka mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) kuanzia mistari mitano (5) hadi nane (8). Kwa watakao bana nywele wanaelekezwa kubana kisogoni kwa kibanio cheusi. Aidha, mwanachuo haruhusiwi kuweka dawa nywele, rasta (dreads), au kubadili nywele rangi (bleaching).

5.3 Mwanachuo haruhusiwi kuwa na kucha ndefu, ndevu na meno yasiyopigwa mswaki.

5.4 Mwanachuo haruhusiwi kupaka rangi za kucha, midomo na kutinda nyusi au kuweka nyusi bandia au kucha bandia.

5.5 Mavazi ya mwanachuo sharti yawe safi na heshima wakati wote.

5.6 Mwanachuo anawajibu wa kuweka matandiko yake na vitu vingine chumbani katika hali ya usafi na unadhifu.

5.7 Mwanachuo anawajibika kufanya usafi wa maeneo, bweni, bwalo la chakula, madarasa, kumbi, vyoo pamoja na maeneo mengine nyakati za asubuhi na siku za mpango kazi. Mwanachuo ambaye hatashiriki usafi atahesabika kuwa ni mtovu wa nidhamu.

5.8 Mwanachuo haruhusiwi kujihusisha na: Matumizi ya vileo na madawa ya kulevya, uvutaji wa sigara au bangi, matumizi ya ugolo au kubeli, vitendo vya ushoga, ubakaji au usagaji, wizi, utapeli, unyang'anyi au kamari ya aina yoyote.

5.9 Wagonjwa wanaelekezwa kwenda zahanati/hospitali kupata ushauri na matibabu. Ruhusa za mapumziko bwenini zitatolewa na mganga, muuguzi, Mratibu wa masuala ya wanachuo au mkufunzi wa zamu.

5.10 Mwanachuo atakayebainika kuwa ana ujauzito atashauriwa kwenda nyumbani kwa sababu za kiafya na miezi sita baada ya kujifungua mwanachuo anaweza kuomba kurejea chuoni kwa kuandika barua kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia kwa Mkuu wa Chuo.

5.11 Mwanachuo atakayebainika kutoa au kujaribu kutoa mimba atakuwa amefanya kosa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za nchi, hivyo atawajibishwa.

5.12 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 5.1 – 5.12 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

**6.0: MAVAZI**

6.1 Mavazi yatakayovaliwa na mwanachuo wakati wote Chuoni sharti yawe ya heshima, safi na yenye kuendana na masharti kwenye kanuni hizi.

6.2 Mwanachuo analazimika kuvaa sare kamili ya Chuo wakati wote na mahali popote (ndani na nje ya chuo) katika kipindi chote cha masomo (semista/muhula) ; isipokuwa wakati wa kazi za nje, nyakati za jioni baada ya masomo, au siku za mapumziko ndani ya chuo.

6.3 Mwanachuo anatakiwa kuvaa kitambulisho chake shingoni wakati wote awapo chuoni au nje ya chuo kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma.

6.4 **SARE KWA WANAUME**

6.4.1 Suruali ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi, itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.

6.4.2 Shati liwe buluu bahari (light blue) mikono mirefu.

6.4.3 Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) au nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.

6.4.4 Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.

6.4.5 Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo).

6.4.6 Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe na ‘track suit’ ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe wakati wa michezo tu.

6.4.7 Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, vilaka, na pete (zisizo za ndoa) na vingine vinavyofanana na hivyo hauruhusiwi.

6.4.8 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 6.4.1 – 6.4.5 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo**.**Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo kabisa.**

6.5 **SARE KWA WANAWAKE**

6.5.1 Sketi rinda boksi ya buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi zenye urefu unaozidi magoti na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.

6.5.2 Shati iwe ‘light blue’ mikono mirefu na tai ndefu ‘dark blue’ au nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.

6.5.3 Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, na soksi ndefu nyeupe.

6.5.4 Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) mistari mitano (5) hadi nane (8) au kubanwa kisogoni kwa kibanio cheusi.

6.5.5 Mwanachuo atakayependa kujisitiri kwa vazi la hijab anaelekezwa kumwona mlezi wake wa kike chuoni au Mkuu wa Chuo kwa maelekezo bayana.

6.5.6 Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe na ‘track suit’ ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.

6.5.7 Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, sketi fupi, nguo zenye mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete (isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.

6.5.8 Uvaaji wa mavazi yasiyokubalika katika kanuni 6.5.7 utapelekea mavazi hayo kuchukuliwa na kuhifadhiwa ofisi ya Mratibu wa masuala ya wanachuo na kufuatiwa na adhabu ya papo kwa papo. Mavazi yaliyoshikiliwa yatarejeshwa kwa mwanachuo atakapomaliza mafunzo.

6.5.9 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 6.5.1 – 6.5.6 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi utapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

## 7.0: RUHUSA

7.1 Mwanachuo atakayetaka kutoka nje ya mipaka ya Chuo kwa shughuli binafsi au za ofisi, atapaswa kujaza fomu ya ruhusa kutoka kwa Mkufunzi wa zamu isipokuwa siku itakapotolewa ruhusa ya jumla.

7.2 Ruhusa zitakazopelekea mwanachuo kulala nje ya chuo zitatolewa na Mkuu wa Chuo kupitia Ofisi ya Masuala ya Wanachuo.

7.3 Mwanachuo anaelekezwa kutoa taarifa kwa kiongozi wa bweni au mkufunzi wa bweni au Mratibu wa masuala ya wanachuo juu ya mwanachuo mwenzake ambaye hayupo Chuoni au hakulala bwenini bila ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Chuo.

7.4 Muda wa mwisho wa mwanachuo kumtembelea mwanachuo mwenzake bwenini wakati wa usiku ni saa nne usiku.

7.5 Ruhusa ya jumla kwa wanachuo itatolewa siku ya Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za Sikukuu kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni wakiwa wamevaa sare za Chuo. Aidha, ruhusa itatolewa kwa waamini wa dini ya kiislam siku ya Ijumaa kati ya saa 6:00 mchana mpaka saa 8:00 Alasiri.

7.6 Siku za Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu ambapo hutolewa ruhusa ya jumla kwa wanachuo kutoka nje ya Chuo, kutakuwa na ‘roll call’ saa 11:30 jioni ambayo kila mwanachuo lazima ahudhurie. Aidha ‘roll call’ inaweza kuitishwa wakati wowote itakapoonekana inafaa.

7.7 Mwanachuo anapotoka chuoni atumie njia zilizo rasmi za usafiri kama vile kufuata barabara au usafiri wa umma.

7.8 Mwanachuo hataruhusiwa kutembelea klabu za pombe, kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni, nyumba/majengo ya michezo ya kamali na michezo ya kubashiri wakati wa mafunzo. **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 7.1 – 7.8 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

## 8.0: TAALUMA

8.1 Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufuata ratiba ya Chuo itakayoanza saa 11:30 asubuhi na kumalizika saa 4:00 usiku.

8.2 Mwanachuo anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na vipindi vya muda wa ziada.

8.3 Mwanachuo anawajibika kuwahi na kukaa darasani muda wote wa masomo.

8.4 Iwapo mwanachuo atakuwa hana kipindi kwa mujibu wa ratiba ya masomo atapaswa kuwa darasani, maktaba au chumba cha TEHAMA au eneo lingine kwa ruhusa maalumu.

8.5 Mwanachuo anatakiwa kushiriki kikamilifu na kuonesha jitihada katika masomo yote yanayotolewa katika kozi anayosoma, kuhudhuria darasani, kufanya majaribio na mitihani yote.

8.6 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 8.1 – 8.5 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**9.0: CHAKULA**

9.1 Huduma ya chakula itatolewa kwa Mwanachuo aliyesajiliwa na kufuata utaratibu wa utoaji wa chakula.

9.2 Milo yote lazima iliwe kwenye Bwalo la chakula isipokuwa kwa kibali maalum. Mwanachuo haruhusiwi kupeleka chakula Bwenini.

9.3 Mwanachuo haruhusiwi kupika au kuwa na Vifaa kama jiko, 'heater', sufuria na kisu Bwenini au mahali pengine popote. Aidha, mwanachuo ni lazima kula chakula kilichopikwa chuoni. Ni marufuku kwa mwanachuo kula au kuingiza ndani ya chuo chakula cha mitaani.

9.4 Mwanachuo haruhusiwi kumkaribisha mtu yeyote kula chakula cha Chuo bila kupewa kibali maalum na Mkuu wa Chuo au mtu anayehusika.

9.5 Mwanachuo haruhusiwi kuingia bwaloni na viatu vya wazi (makobazi), kandambili, kaptula, kanga, vesti, gauni ya kulalia, skafu, taulo, kofia, na vitu vinavyo fanana na hivyo.

9.6 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 9.1 – 9.5 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**10.0: UTUNZAJI WA MALI ZA CHUO**

10.1 Mwanachuo anaelekezwa kutumia mali ya Umma vizuri kama umeme na maji ili kuimarisha uendelevu na kuepuka gharama zisizo za lazima.

10.2 Kiongozi wa bweni na wanabweni wana wajibu wa kutunza mali zote za bweni na nyaraka muhimu.

10.3 Mwanachuo haruhusiwi kufanya marekebisho au maunganisho ya mtandao, umeme au maji pasipo ruhusa maalum.

10.4 Mwanachuo haruhusiwi kuandika, kuchora au kupaka rangi katika majengo au vifaa mbali mbali pasipo maelekezo maalumu.

10.5 Mwanachuo anaelekezwa kurejesha kwa wakati mali ya Umma iliyoazimwa.

10.6 Wizi wa mali ya umma au mali ya mtu mwingine ni kosa la kinidhamu kwa mujibu wa kanuni hizi na jinai kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi.

10.7 Milango ya majengo na mabomba za maji yafungwe na Taa zizimwe wakati ambapo havitumiki. Viongozi wa mabweni watawajibishwa kwa kutokutekeleza kanuni hii.

10.8 Mwanachuo haruhusiwi kujihusisha na biashara yoyote chuoni.

10.9 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 10.1 – 10.8 anaweza kupewa adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua), kulipa gharama yote ya uharibifu alioufanya au kusababisha au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hizi kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**11.0: HABARI NA MAWASILIANO**

11.1 Mawasiliano yafanyike kwa kuzingatia daraja/hadhi ya mtu mfano: kiongozi, mkufunzi, wafanyakazi wasio wakufunzi, n.k. Lugha ya matusi, kejeli, dharau, dhihaka na lugha za kudhalilisha hazitavumiliwa.

11.2 Mawasiliano yote rasmi nje ya Chuo ni lazima yafanywe kupitia ofisi ya Mkuu wa Chuo. Hii ni pamoja na mialiko ya michezo, mikutano, semina, warsha baina ya wanachuo na watu au jumuiya ya nje.

11.3 Taarifa ya msiba, ugonjwa na taarifa nyingine muhimu kutoka nyumbani zinazomuhusu mwanachuo ziwasilishwe Ofisi ya Mratibu wa Masuala ya Wanachuo na mtoa taarifa.

11.4 Wanachuo hawaruhusiwi kukusanyika au kufanya mkutano bila idhini ya Mkuu wa Chuo.

11.5 Mwanachuo haruhusiwi kupiga kelele, kufungulia redio au chombo chochote cha muziki kwa sauti ya juu kiasi cha kuleta usumbufu kwa majirani zake.

11.6 Mwanachuo au mtu yeyote yule haruhusiwi kupiga picha au kurekodi taarifa yeyote na kurusha katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii bila idhini ya mhusika au Mkuu wa Chuo.

11.7 Matumizi yasiyo rasmi ya vifaa vya kielektroniki kama vile simu kwenye vyumba vya mitihani, darasani au kwenye mikusanyiko maalumu hayaruhusiwi bila idhini ya Mkuu wa Chuo.

11.8 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 11.1 – 11.7 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**12.0: ULINZI NA USALAMA:**

12.1 Mwanachuo anatakiwa kutii tahadhari zote za ulinzi na usalama.

12.2 Mwanachuo anatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa Chuo mara tu kunapotokea viashiria vya hali au tukio lisilo la kawaida.

12.3 Mwanachuo anawajibu wa kuwa mlinzi wa mali yake binafsi na mali ya umma.

12.4 Mwanachuo haruhusiwi kushawishi, kuongoza, kushiriki mgomo na maandamano ya aina yeyote bila kibali.

12.5 Mwanachuo haruhusiwi kumiliki aina yoyote ya silaha chuoni.

12.6 Mwanachuo hatakiwi kutoa matamshi yanayopelekea taharuki na au chuki na kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo.

12.7 Mwanachuo hatakiwi kugombana na au kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo.

12.8 **Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni 12.1 – 12.7 atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua au adhabu nyingine inayofanana na hizo.Kujirudia kwa uvunjaji wa kanuni hii kutapelekea mwanachuo kupewa kazi ngumu, kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.**

**13.0: Muhtasari**

Sheria na kanuni hizi zinapaswa kusomwa pamoja na sheria nyinginezo kama vile sheria za mitihani na maelekezo halali ya maeneo mengine. Uvunjaji wa taratibu zozote zilizopo utakuwa ni kosa na hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa uzito unaostahili. **Timiza wajibu, tii sheria bila ya shuruti**.

...........................

**Catherine T. Kimboka**
**Mkuu wa Chuo**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU SONGEA
S L.P. 189
SONGEA